



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI

MSIMAMIZI WA UCHAGUZI

HALMASHAURI YA MOROGORO

JIMBO LA MOROGORO MJINI

Kumb. Na. R.10/MMC-27/122

Tarehe 21/09/2020

**TANGAZOLA NAFASI ZA KAZI ZA MUDA**

Msimamizi wa Uchaguzi Jimbo la Morogoro MJini kwa kuzingatia kanuni ya 14 ya Kanuni za Uchaguzi wa Rais na Wabunge za Mwaka 2020 na kanuni ya 12 ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa (Uchaguzi wa Madiwani) za mwaka 2020, anakaribisha maombi kutoka kwa Watanzania wenyewe sifa na uwezowa kujaza nafasi za Wafendaji wa Uchaguzi Mkuu utakaofanyika tarehe 28 Oktoba, 2020 kama ifuatavyo:

1. MSIMAMIZI WA KITOO CHA KUPIGIA KURA
2. MSIMAMIZI MSAIDIZI WA KITOO CHA KUPIGIA KURA
3. KARANI MWONGOZAJI WAPIGA KURA

**A. SIFA ZA WAOMBAJI WA NAFASI YA MSIMAMIZI AU MSIMAMIZI MSAIDIZI WA KITOO CHA KUPIGIA KURA**

- (a) Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi;
- (b) Asiwe shabiki au kiongozi wa chama cha siasa;
- (c) Awe mwadilifu, mtiifu na mwenye akili timamu;
- (d) Awe amemaliza elimu ya kidato cha nne (4) au zaidi na anaweza kusoma na kuandika vizuri. Pia, anayeweza kuyaelewa Maelekezo ya Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura; na
- (e) Ikiwezekana awe mkazi wa kata ambayo anaomba.

**B. SIFA ZA WAOMBAJI WA NAFASI ZA KARANI MWONGOZAJI WA WAPIGA KURA**

- (a) Awe raia wa Tanzania mwenye umri wa miaka 18 au zaidi;
- (b) Awe mkazi wa kata ambayo atafanya kazi ya kuongoza wapiga kura;
- (c) Ikiwezekana awe mpiga kura wa kituo anachofanya kazi;

- (d) Awe mwadilifu, mtiifu na mwenye akili timamu;
- (e) Awe na elimu isiyopungua kidato cha nne na anayeweza kusoma na kuyaelewa Maelekezo kwa Makarani Waongozaji Wapiga Kura; na
- (f) Asiwe shabiki au kiongozi wa chama cha siasa.

**C. MALIPO**

Malipo yatakuwa kama ifuatavyo:-


- i. Msimamizi wa Kituo siku ya Uchaguzi atalipwa posho ya Tzs. 35,000 kwa siku kwa muda wa siku mbili, posho ya chakula Tzs 15,000 kwa siku moja na nauli Tzs 20,000;
- ii. Msimamizi Msaidizi wa Kituo atalipwa posho ya Tzs. 30,000 kwa siku kwa muda wa siku mbili, posho ya chakula Tzs 15,000 na nauli Tzs 20,000; na
- iii. Karani Mwongozaji Wapiga Kura atalipwa posho ya Tzs 30,000 kwa siku moja na posho ya chakula Tzs 15,000.

**D. MASHARITI YA JUMLA KWA KAZI ZOTE**

- Waombaji waambatishe maelezo binafsi (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuamikaa pamoja na majina ya wadhamini (Referees) wawili.
- Maombi yote yaambalanena Vyeti vya taaluma, nakala za Vyefi vya Kidato cha Nne, Kidato cha Sitaa au kuhitiinu mafunzo kwa kuzingatia sifa kwa mujibu wa Tangazo hili.
- Waombaji waambatishe picha mbili 'Passport size' za hivi karibuni.
- Waombaji ambao tayari ni Watumishi wa Umma wapitishe barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa waajiri wao.
- Waombaji watakaowasilisha taarifa na sifa za kugushi watachukuliwa hatua za kisheria.
- Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 27 Septemba , 2020.

Anuani ya kutuma maombi ya kazi ni:-

Msimamizi wa Uchaguzi,  
Jimbo la Morogoro Mjini,  
S. L. P. 166,  
MOROGORO

  
SHELLA E. LUKUBA  
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI  
JIMBO LA MOROGORO MJINI

